



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA
KAHAMA

Unapo jibutafadhalitaja:

Kumb. Na. KMC.E.5014/96

03 Novemba, 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi ya Ajira ya Mkataba ya Madereva nafasi Tano (05).

SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania.
- ii. Awe amehitimu Kidato cha IV na awe na Ufaulu wa Daraja la nne na kuendelea.
- iii. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani.
- iv. Awe na leseni ya udereva Daraja C au E ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- v. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha VETA au NIT au Chuo kingine kinachotambuliwa Serikali.

MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA II

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbali mbali kwenye safari za kikazi
- iii. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbali mbali.
- iv. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- v. Kufanya usafi wa gari.


MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA

- i. Awe na umri ya miaka 18-45 (Ambatanisha cheti cha kuzaliwa)
- ii. Waombaji waambatishe vivuli vya Vyeti vyao vya Elimu na taaluma pamoja na maelezo binafsi (CV).
- iii. Katika barua ya maombi, weka Namba yako ya simu inayopatikana muda wote.
- iv. Barua zibandikwe picha mbili (2) - Passport size.
- v. Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili.
- vi. Mwisho wa kupokea maombi ni **14 Novemba, 2023** saa **9:30** alasiri.
- vii. Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
81Barabara ya Boma,
37305 Malunga,
S.L.P 472,

KAHAMA-SHINYANGA

Limetolewa na:


Anderson D. Msumba

**MKURUGENZI WA MANISPAA
KAHAMA.**

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA